

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

621

KISWAHILI

Mwaka: 2022

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** kwenye chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili anapata ujuzi gani? Taja kwa mtiririko kwa kuanza na ujuzi wa kwanza hadi wa nne.
2. "Fikiri huvutiwa sana na wahusika katika hadithi mbalimbali anazosisoma." Chambua kwa ufupi wahusika wanne waliomo katika hadithi hizo.
3. Chagua neno sahihi kutoka katika orodha ya maneno yaliyo katika kisanduku kisha kamilisha muundo wa sentensi zinazofuata.

hizi, kwa, ingawa, ni, ndio, baadaye, isipokuwa, nje ya, au, hawa, kama, na, naye, baada ya, nae, huyu.

- (a) Tulikutana naye \_\_\_\_\_ akaondoka.
  - (b) Watu \_\_\_\_\_ waliingia nchini mwaka juzi.
  - (c) Juma hakufaulu mtihani \_\_\_\_\_ alisoma kwa bidii.
  - (d) Nitanunua gari \_\_\_\_\_ kujenga nyumba.
  - (e) Mwanafunzi alikimbia kwa kasi \_\_\_\_\_ mshale.
  - (f) Baba anakula wali \_\_\_\_\_ kijiko.
  - (g) Mama yangu \_\_\_\_\_ mpishi mzuri sana.
  - (h) Sisi tutasafiri pamoja \_\_\_\_\_.
4. Ni mambo gani yanayotakiwa kuzingatiwa ili kusaidia utungaji wa maandishi kuwa bora zaidi? Taja mambo manne.
  5. Kwa kutumia mfano kwa kila moja, tofautisha aina za maneno zifuatazo:
    - (a) Kiwakilishi na Kivumishi
    - (b) Kiunganishi na Kihusishi
  6. Mwalimu anayetumia onesho mbinu wakati wa kufundisha somo la Kiswahili hupata manufaa gani? Eleza kwa ufupi kwa kutumia hoja nne.
  7. Picha na michoro inayopaswa kuwemo katika kitabu cha kiada cha mwanafunzi wa shule ya msingi inatakiwa kuwa na sifa gani? Eleza kwa ufupi sifa nne.

8. Mwalimu anaweza kupata zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kwa namna gani? Ainisha namna nne.
9. Mwalimu Kibonde amepanga kuwafundisha wanafunzi wake wa Darasa la Tano somo la kusoma kimya. Fafanua kwa ufupi hatua nne atakazopaswa kuzifuata wakati wa kufundisha somo hilo.
10. Je, ni changamoto gani zinaweza kujitokeza iwapo mwalimu atatumia mbinu ya kualika mgeni katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili? Chambua kwa ufupi changamoto nne.

### **SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. Mwandikie barua Alfa Mkanjunju wa S.L.P 18 Mwanza ambaye ni rafiki yako, umweleze kuwa umehamia Katavi kikazi. Jina lako liwe Mafuniko Mengi wa S.L.P 218, Katavi.
12. Mwalimu anayefundisha stadi za kuzungumza na kusikiliza hukabiliana na changamoto gani? Kwa kutumia mifano dhahiri, fafanua changamoto tatu na namna ya kukabiliana nazo.
13. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili una faida gani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji? Eleza faida tano.
14. "Taaluma na utalaamu wa mwalimu hautoshi kumfanya mwalimu afundishe bila andalio la somo." Tumia hoja tano kuthibitisha kauli hiyo.